CHRISTIAN COUNCIL OF TANZANIA
JUMUIYA YA KIKRISTO TANZANIA
CCT CHURCH HOUSE

Tel: 026 232 4445
Along Hospital Road
Between 8th and 9th Road
Postcode 41103
P.O. Box 1454
Dodoma,
TANZANIA.

**YOUR REF. No.**

**OUR REF. No.**
**CCT/GS/GOVT/38**

**DATE:**
**30.09.2025**

**YAH: TAARIFA KWA UMMA**

Rejea kichwa cha habari hapo.

Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT) inapenda kuujulisha umma kuwa barua yenye Kichwa **YAH: MSIMAMO WA PAMOJA KUHUSU UCHAGUZI MKUU TANZANIA** ya **Tarehe 21.07.2025** iliyoelekezwa kwa Waheshimiwa Maaskofu Wakuu na Wanachama wa Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT) kuwa **SIO BARUA HALALI** inayotoka kwenye mamlaka za CCT.

Jumuiya inao utaratibu wake wa kufanya maamuzi na kuyawasilisha kwa Wanachama wake na Umma. Jumuiya inawataka Wananchi kuheshimu taratibu za Taasisi yetu na kutokutumia jina lake kwa jumbe ambazo sio rasmi. Aidha Jumuiya haitasita kuchukua hatua za kisheria kwa mtu, kikundi au taasisi yoyote itakayobainika kukiuka taratibu hizi.

Jumuiya inaendelea kutoa wito kwa Wanachama wake na Watanzania kwa ujumla kuendelea kuliombea Taifa Haki, Amani na Utulivu katika kipindi hichi cha kuelekea Uchaguzi Mkuu.

**"Haki huinua Taifa; Bali dhambi ni aibu ya watu wo wote" Mithali 14:34**

Katika Utumishi,

Christian Council of Tanzania
P.O. Box 1454 - Dodoma
Tanzania

Godlisten Moshi
**KAIMU KATIBU MKUU**

**Nakala:** Mwenyekiti wa Jumuiya ya Kikristo Tanzania
Maofisa wa Jumuiya ya Kikristo Tanzania